# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**MANG'U HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

**MANG'U HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016**

**102/3**

**KARATASI YA 3**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. **MAJIBU YA SHAIRI**

(a) Nafsineni ni mwananchi/raia/mzalendo/mtetezi wa haki za binadamu/za wanyonge.

(b) (i) Tabdila – Kuleta urari wa vina mfano: usitatanizwe, wanaturararuwa.

(ii) Inkisari – Kuleta urari mizani mfano: aso.

(iii) Utohozi – Hi kuleta urari wa vina na mizani mfano: noleji.

(c) (i) Sakarani – Shairi ni mseto wa bahari kadha mfano tathmina, utatu, ukaraguni n.k.

(ii) Kikwamba neno longa linaanzia na kurudiwa kila ubeti.

(iii) Ukaraguni – Vina vya ukwapi na utao vinabadilika kila ubeti.

(iv) Mathnawi – Shairi limegawika vipande viwili kila mshororo.

(v) Kikai – Mizani katika utao ni michache (6) ilhali. Mizani ya ukwapi ni mingi (8).

(vi) Sabilia – Halina pambio bali lina kituo.

(d) (i) Anafora – huu ni urudiaji/uradidi neno longa imerudiwarudiwa.

(ii) Usambamba wa kiusawe – neno longa lina maana sawa na nena, sema, zungumza, ongea, kuli, tamka na ambayo yametumiwa kwenye shairi.

(iii) Usambamba wa kifahiwa/dhamira – mtunzi anadhamiria kusisitiza haja ya kuwaumbua na kuwasuta wabunge walafi na wenye kuzua balaa.

(iv) Tabaini - Si uasi si tenge si noma.
- Si kiwara si medani

(v) Jazanda – Mabubu – Wenye kujitia hamnazo
- Kishindo cha funo – tishio hafifu/tishio la nyamarero

(e) Toni – ghadhabu/hasira

(f) Adhidadi – pole/taratibu

(g) Afwaji – kaumu/halaiki/umati wa watu

2. **MSTAHIKI MEYA**

(a) Maneno ya Siki✓ akimwambia Diwani III✓Nyumbani✓ kwa Meya wakiwa wamestarehe barazani. Siku alikuwa ameenda kumtembelea kumwomba amshawishi Meya aboreshe hali ya maisha✓ hasa kwa kuboresha hospitali (kuleta dawa). (1 x 4)

(b) ***JAZANDA*** (1 x 1)

Maana: Ingawa wote wawili ni binamu, huwasikilizani wala kushirikiana (1 x 1)

(c)

– Anaishi maisha ya kifahazi raia wakikosa mahitaji ya kimsingi k.m. Chukula, dawa n.k.

- Alijilimbikizia mali huko raia wakiteseka.
- Hawajibiki kazini/hajali kuhusu utenda kazi.
- Ana kiburi.  Hataki kuitwa kwa jina na Siki.
- Anadharau na kupuuza wawkilishi wa wafanyikazi kwa kuwaambia wanampotezea wakati.
- Anapuuza ushauri wa Siki na Diwani III na kusikiza wa Bili, Diwani I na Diwani II.
- Hashughulikii malalamishi ya wafanyikazi.
- Ni fisadi: Aunga mkono wizi wa fimbo ya Meya na kuiuza ili wafaidike peke yao.
- Anatumia udikteta kuidhinisha baadhi ya maamuzi ya kujinufaisha pamoja na marafikize.
- Atumia askari kunyamazisha wanaogoma.
- Amlipa mhubiri ili amwombee yeye na baraza.  Maombi hayawajali wengine.
- Kutumia Mayors Act dhidi yaw engine.

(Hakiki hoja zingine zinazo – 7 x 2 = 14 onyesha Meya yu na mamlaka zaidi).

3. Thibitisha ukweli wa msemo kuwa sikio la kufa halisikii dawa kwa mujibu wa tamthilia ya Mstahiki Meya.

(i) Meya alikataa kusikiliza ushauri wa Siki kuwa watu waliomchagua wanamlilia awatatulie matatizo yaliyowakabili hasa kwa kuwaongezea mshahara.

(ii) Siki alimsihi Meya anyooshe mengi yasiyonyooka ili watu wasilipuke lakini Meya hakumsikia; aliendelea na maovu na mapuuza yake.

(iii) Siki alimwambia Meya kuwa kuna watu wanaokufa kwa ukosefu wa dawa na njaa lakini Meya alimpuuza na kusema kuwa Baraza analoongoza ni dhabiti kuliko mengine jirani.

(iv) Meya anapoamrisha nyimbo za kizalendo ziimbwe kabla na baada ya vipindi marufu ili kuamsha uzalendo, Siki anamshauri kuwa nyimbo hazitawashibisha na kukata kiu ya uhitaji wa watu lakini Meya hakulitilia maanani.

(v) Siki anapomtahadharisha kuwa kulipisha watu matibabu hospitalini kunapinga mpango wa afya bora nay a bure Meya anasema malengo yale ni upuuzi.

(vi) Siki pia alimtahadharisha Meya hatari ya kufuata maamuzi ya mataifa fadhili bila kushirikisha watu wao kwani huo ni ukoloni mamboleo. Badala ya kusikiliza ushauri huu Meya anamwita mlinzi wake amfukuze pale.

(vii) Diwani III alimwonyesha Meya hatari ya kuongezea madiwani mshahara na kuwaacha wafanyakazi wengine lakini akapuuza.

(viii) Meya pia anapuuza ushauri wa Diwani III kuwashughulikia wafanyakazi ili kuepuka tisho la mgomo. Anaonelea kuwa watalazimishwa na mahitaji ya kila siku kusitisha mgomo na kurudi kazini.

(ix) Meya pia anapuuza ushauri wa Diwani III kuwadhamini wafanyakazi kwani wanawahitaji, badala yake anasema hata wakigoma wataajiri wengine.

(x) Meya anapuuza ushauri wa Diwani III kuwa kuchukua mikopo kwa wafadhili kungewaachia vizazi vijavyo mzigo wa kufidia. Meya haoni haja ya kujali ya badaye.

(xi) Kwa muda Meya anaepuka kuzungumza na wafanyakazi kuhusiana na hali yao ili kuzima mgomokwa kuamini kuwa uhitaji ungewafanya warudi kazini.

(xii) Anapokubali kuongea na viongozi wa wafanyakazi haonekani kutilia maanani mazuungumzo yao na kwa hivyo wanamwacha.

(xiii) Mapuuza haya yanasababisha mgomo mkubwa wa wafanyakazi uliosababisha wageni aliotarajia kutoweza kuhudhuria mkutano.

(xiv) Yeye na madiwani wake waaminifu wanakamatwa na polisi na kupelekwa katika Makao Makuu kueleza hali ya mambo.

(xv) Hatimaye alitambua kuwa baadhi ya madiwani waliojifanya waaminifu walimdanganya.

(xvi) Anajuta na kusema ni heri angemsikiliza Diwani III (Bwana Uchumi na Kazi) kwa kutambua kuwa ingawa hakupenda maoni yake anaona yalikuwa ya kweli.

Zozote 10 x 2 = 20

4. **KANDA LA USUFI**

(a) Maneno haya ni ya <u>msimulizi</u>.
Arejelea <u>Sela</u> na <u>Masazu</u> wakati Sela alijitolea kumsaidia.
Masazu aliyejifanya mgonjwa ikiwa mbinu ya kumnasa.
Ni katika <u>shule ya Askofu Timotheo</u> ambako wanafunzi kutoka shule mbalimbali walikuwa wameenda kwa mashindano ya muziki. (4 x 1 = 4)

(b)

- Wasichana wa Askofu Timotheo kupata mimba na kufukuzwa.
- Baadhi ya wanafunzi k.m. Masazu hutoka shuleni mwao kwenda za wasichana sio kwa sababu za tamasha bali kupata wachumba.
- Wasichana wajawazito hukosa makini darasani.
- Wavulana nao hukosa kutia bidii kwa sababu ya mawazo k.m. Masazu alikosa kupita vizuri.
- Wanafunzi kutumia muda mwingi kuandikiana barua za mapenzi badala ya kusoma.

(5 x 2 =10)

(c)

- Sela na Masazu kufika kwenye kliniki na kukutana na Sista akitoka wakakutania mlangoni.
- Sista 'aliyemsaidia' Masazu ndiye bado alimpima Sela mjamzito alikuja kufukuzwa shule.
- Kutumbukia kwa Sela majini na hivyo kutomfikisha nyumbani mtoto waliyemjia.
- Mvua kubwa kunyesha usiku wa kumtorosha Kadogo. (3 x 2 = 6)

5. **MAJAZI**

Sudi – maana yake ni bahati njema.
Sudi alikuwa na bahati kuokotwa na Bi. Mkubwa pipani kabla hajakata roho.
Sudi alikuwa na bahati ya kulelewa na Bi. Mkubwa vizuri.
Sudi alikuwa na bahati ya kuelimishwa.
Sudi alikuwa na bahati ya kupata kazi nzuri.
Sudi alikuwa na bahati ya kurithishwa nyumba.
Sudi alikuwa na bahati ya kumpata mamake mzazi bila kumtafuta. (7 x 2 = 14)
Kudura – Maana yake ni nguvu za Mwenyezi Mungu.
Ni kudura mama mzazi wa Sudi kupata kazi.
Ni kudura kuwa anayemwajiri kazi ni mwanawe.
Ni kudura kupata mwanawe aliyemtupa pipani zamani. (3 x 2 = 6)

6.

- Jamii mpya ambayo haitakuwa na unyanyasaji k.v. kunyang'anya wanyonge mali yao/mashamba yao kama alivyofanya Mtemi Nasaba Bora kwa familia za Amani na Imani.
- Jamii mpya ambayo haitakuwa na ufisadi k.v. Mtemi Nasaba Bora alivyohonga wakuu serikalini ili mwanawe madhubuti aajiriwe katika jeshi.
- Jamii inayotekeleza haki siyo yenye kufunga jela watu wasio na hatia kama alivyofungwa Yusufu ami yake Amani kupitia mipango ya Mtemi.
- Jamii isiyotekeleza mauaji kwa watu wasio na hatia kama alivyouawa Chichiri Hamadi babaye Amani kupitia njama iliyohusisha Mtemi.

- Jamii isiyo na ukatili k.v. Mtemi Nasaba Bora alivyotupa kitoto chake kichanga mlangoni pa Amani. Alivyompiga Amani nusura amuue, alivyokataa kushughulikia matibabu ya Bob D. J baada yakung'atwa na mbwa wake n.k.
- Jamii yenye viongozi waliowajibika na kutumika wananchi sio kujifaidi na kuwakandamiza kama alivyokuwa Mtemi Nasaba Bora.
- Jamii inayotambua na kuauni mashujaa wa zamani k.v. Mzee Matuko Weye alivyopigana vita vikuu vya dunia na Chwechwe Makweche aliyechezea Tomoko soka ya kimataifa.
- Jamii isiyopuuza walemavu Mwalimu Majisifu hakuthamini watoto wake wane walemavu lakini Imani alimfanya abadilike.
- Jamii isiyo na uzinifu na yenye ndoa zilizo na uaminifu.  Nasaba Bora alitembea na wasichana wadogo kama Lowela Maozi.
- Jamii yenye vijana wanaoweza kungoja hadi waoane kabla ya kushiriki mapenzi kama wanavyofanya Amani ns Imani.
- Jamii yenye waandishi wanaochapishiwa miswada yao ikiwa mizuri sio inayoibwa na kutumika na wengine.
- Jamii yenye watu ambao hawataendelea kunyamaza wakinyanyaswa lakini watajikombokoa kwa kufanya mapinduzi k.v. Amani na Madhubuti.
- Jamii yenye kujali masilahi ya wengine na kugawa rasilimali zilizopo kwa maskini kama alivyofanya Amani kwa Matuko Weye, Bob D.J na wengine.
- Jamii yenye msamaha na isiyo na kisasi.  Amani alikuwa na nafasi amdhuru Mtemi Nasaba Bora lakini akaamua alipe ubaya kwa wema.
- Jamii yenye huduma bora za kimsingi kwa wananchi k.m afya sio kama vile Zahanati ya Nasaba Bora ilivyokuwa. Zozote 10 x 2 = 20

7. (a) Jadili mambo yaliyomshitua Mtemi Nasaba Bora kuhusiana na barua na gazeti alizozipokea siku hiyo.

- Hakuona picha yake katika gazeti la Tomoko Leo kama ilivyokuwa wakati nduguye Mwalimu Majisifu alikuwa mhariri wa gazeti hilo licha ya kutoelewana kwao.

- Katika barua aliyopokea mtoto wake madhubuti aliyekuwa masomoni.  Urusi alimwarifu juu ya kurejea kwake nyumbani na angetaka mpango wa kumtafutia ajira jeshini au popote uisitishwe, kwa sababu hataki ajira inayotokana na mlungula.

- Madhubuti pia alisema kuwa alitaka kusimama kwa miguu yake mwenyewe apate au akose kwa kustahiki au kushtahili kwa sababu ya jadi yake.

- Madhubuti alimwambia babake alikuwa amechoka na ingawa alimpenda kulikuwa na vitendo vyake ambavyo hakuwa akivipenda.

- Mtemi Nasaba Bora alipomaliza kusoma barua alikasirika na kugonga meza kwa kuona kuwa madhubuti hajui dunia inavyozanguka.

- Pia alikasirika kwa kuona Madhubuti alivyokuwa amejitambulisha na mamake(Madhubuti Zuhura) badala ya kujitambulisha naye kama baba yake. (5 x 2 = 10)

(b) **Onyesha jinsi Madhubuti alivyoendeleza uasi dhidi ya babake**.

- Katika barua aliyomwandikia babake alipokaribia kurudi nyumbani alitaka mipango ya kutafutiwa kazi jeshini au popote isitishwe kwa sababu hukutaka kazi iliyotokana na mlungula.

- Madhubuti alimwambia babake kuwa ingawa alimpenda kulikuwa na vitendo vyake ambavyo hakupenda.

- Madhubuti alimaliza barua yake kwa kujiita Madhubuti Zuhura badala ya kujitambulisha na babake.

- Alipendana na kushirikana na mfanyikazi wao Amani kwa sababu mitazamo yao ilishabihiana. Hatimaye alihamia kibandani alimokaa Amani.

- Madhubuti alichukia vitendo vya babake vya kupoka, kupiga pute, kulimbikiza mali haramu na kuhalalisha haramu kwa sababu vilifanya bara la Afrika kuchekwa katika kila pembe ya dunia.

- Alimwomba Amani ashirikiane naye katika kuwazidua watu kwa lengo la kukomesha udhalimu kuanzia pale kwao wanapofanyiwa udhalimu na baba yake.

- Madhubuti alifuata kwa kukubali babake ampeleke masomoni ng'ambo kwa pesa alizowaitisha watu kwa nguvu ingawa alikuwa amefaulu kuingia katika Chuo Kikuu pale nyumbani kwao.

- Anahiari kujiua kinasaba ili azaliwe upya na asiwe na uhusiano wowote na Nasaba ya Mtemi Nasaba Bora.

- Madhubuti alikubaliana na Amani waongoze mapinduzi kwa tahadhari wasije wakatoa viongozi dhalimu na kuingiza mwingine dhalimu zaidi.

- Madhubuti alipopata ajira mjini Songoa alianza kuchunguza jinsi babake alivyopata kumiliki mashamba mengi makubwa.

(5 x 2 = 10)8.

(a)

- Maigizo ni sanaa ya mazungumzo yanayoambatana na matendo.
- Ni hali ambapo watendaji hutenda na huiga matendo ya watu au viumbe katika jamii.

(1 x 2 = 2)

(b)

- Hutolewa au huigizwa mbele ya hadhira.

- Uigizaji huhitaji uwanja maalum wa kutendea au mandhari.

- Hufangamana na shughuli za kijamii kama vile utambaji wa hadithi na sherehe.

- Sharti kuwe na tendo la kuigizwa.

- Waigizaji huvaa maleba yanayooana na hali wanazoigiza.
- Maigizo huiga hali ya maisha ya jamii kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kwa nia ya kuonyesha mafanikio, udhaifu na migogoro katika nyanja za maisha.
- Huwa na muundo mahsusi wa mtiririko wa matukio.
- Yanaweza kuambatana na ngoma pamoja na uimbaji wa nyimbo au ukariri wa tungo za kishairi.
- Hutumia lugha yenye ufundi mkubwa.
- Wakati mwingine hutumia ishara. Zozote (5 x 2 = 10)

(c) **Dhima ya michezo ya watoto**.

- Hukuza kipawa cha uigizaji miongoni mwa watoto.
- Hukuza ubunifu.
- Ni nyenzo ya kukashifu matendo hasi ya watu wazima.
- Hutambulisha na kusawiri falsafa ya jamii kuhusu malezi na majukumu ya wanajamii.
- Huwapa watoto ukakamavu na kuwawezesha kujiamini wakiwa wangali wachanga.
- Hukuza utangamano/ushirikiano/umoja.
- Huimarisha uwezo wa kukumbuka.
- Huwawezesha kupata mikakati au maarifa ya kukabiliana na hali mbalimbali katika maisha.
- Huburudisha.
- Huendeleze utamaduni wa jamii husika.
- Huhifadhi historia ya jamii husika. n.k. Zozote (4 x 2 = 8)